k. Yakinisha sentensi ifuatayo: (alama 2)

Usingeacha masomo, usingetaabika vile.

........................................................................................................

l. Unda nomino kutokana na kitenzi –fa- (alama 2)

........................................................................................................

m. Andika katika msemo wa taarifa: (alama 3)

"Leo jioni tutashuhudi mechi ya kukata na shoka." Mati alisema.

........................................................................................................

........................................................................................................

n. Andika vitenzi vifuatavyo katika kauli kwenye mabano: (alama 3)

i. Tembea (kutendeshwa) ..................................................................

ii. Okoa (kutendeta) ..................................................................

iii. Pika (kutendeka) ..................................................................

o. Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa wingi: (alama 2)

Debe hilo litasafirishwa pamoja na nyundo hii.

........................................................................................................

p. Tunga sentensi moja kudhihirisha maana tofauti ya neno **futa** na **vuta.** (alama 2)

........................................................................................................

........................................................................................................

q. Tofautisha sentensi ifuatayo: (alama 2)

Ningalisoma kwa bidii ningalipata mtihani.

Ningesoma kwa bidii ningepita mtihani.

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

r. Andika sentensi ifuatayo bila kutumia 'amba'. (alama 2)

Mwalimu ambaye amewasili anatufunza.

........................................................................................................



**4. ISIMUJAMII (alama 10)**

a) Eleza maana ya dhana zifuatazo: (alama 4)

i. Linguafranka..................................................................

..................................................................

..................................................................

ii. Pijini..................................................................

..................................................................

..................................................................

b) Eleza vikwazo **sita** kwa mawasiliano. (alama 6)

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

........................................................................................................

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

b) Kwa kuzingatia maneno 45-50, eleza athari za mimba za mapema miongoni mwa wasichana kwa kurejelea aya mbili za mwisho (Alama 6, Utiririko 1)

**Matayarisho**

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

**Jibu**

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

## 3. MATUMIZI YA LUGHA

a. Taja sauti mbili zinazotamkiwa mdomoni (alama 2)

.............................................................................................................

b. Toa mifano miwili ya maneno yanayoundwa kwa silabi wazi. (alama 2)

.............................................................................................................

.............................................................................................................

c. Akifisha sentensi ifuatayo ilete maana tatu tofauti: (alama 3)

Watu wanakula nyoka.

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................



d. Huku ukitoa mfano, fafanua dhana ya mzizi wa neno (alama 2)

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

e. Bainisha mofimu katika neno: **aliwanywea** (alama 3)

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

f. Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya ngeli ya YA-YA (alama 2)

.............................................................................................................

.............................................................................................................

g. Andika senstensi ifuatayo katika umoja : (alama 2)

Walowezi waliyanyakua mashamba ya waafrika.

.............................................................................................................

.............................................................................................................

h. Bainisha vivumishi katika sentensi ifuatayo; (alama 2)

Mtoto mwenyewe alienda shambani kufanya kazi yetu.

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

i. Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi. (alama 2)

Beti alishindia tuzo. Beti alishiriki katiki utunzaji wa mazingira.

.............................................................................................................

.............................................................................................................

j. Andika kinyume cha sentensi ifuatayo: (alama 2)

Wasichana watatu wanaingia darasani kwa haraka.

.............................................................................................................

.............................................................................................................

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

e) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika kwenye kifungu (alama 3)

i. Mizani............................................................................................

ii. Halahala.........................................................................................

iii. Watwana..........................................................................................

## 2. UFUPISHO (ALAMA 15)

***Soma Makala yafuatayo kasha ujibu maswali***

Usasa na mabadiliko katika mitindo ya maisha ni miongoni mwa mambo yanayochangia kuongezeka kwa idadi ya wasichana wadogo kupata mimba. Katika jamii ya zamani ya Kenya, msichana ambaye hajaolewa alipata mimba kwa tukizi sana. Lakini maadili ya kungani yamedidimia sana siku hizi na hivyo kujenga mazingira mwafaka ya wasichana kubeba mimba wakiwa wadogo. Imekuwa hali ya watoto kuzaa watoto wenzao. Sambamba ni ongezeko la wasichana wadogo wanaoshika mimba kuondolewa shuleni kwa fedheha inayoambatana na mimba nje ya ndoa.

Usasa umesambaratisha mfumo wa kitamaduni uliohakikisha kwamba akina nyanya wanafunza wasichana mambo ya kiutuuzima. Vivyo hivyo usasa umewatenganisha wavulana na babu zao waliokuwa chanzo cha hekima ya mambo ya kiutuuzima. Wasichana chungu nzima wanazaliwa na kulelewa katika majiji na miji- mbali na nyanya zao, vijana wengine- wavulana kwa wasichana, wameachwa kutapatapa katika bahari ya maisha bila mwelekezo kwa vile wazazi wao wenye haya wanashindwa kuwakabili na kusema nao kuhusu mambo ya ngono. Wanabaki kuokotaokota porojo na hekaya za marika zao, majarida ya kutilika shaka, wavuti na sinema zisizoaminika. Vyanzo hivi vya maelezo kuhusu ngono vinachochea harara katika miili ya vijana hao wanaopitia mabadiliko ya kubalehe.

Utukuzaji wa ngono unatilia shadda na kugeuza ngono kuwa bidhaa ya kibiashara. Hili huchangia dhana potovu kwamba ngono si tu chanzo cha ureda bali chanzo cha kipato. Baadhi ya wasichana wanalazimika kuchuuza miili yao ili kusaidia uzumbuaji wa riziki kwa familia zao. Mara nyingine tokeo ni kupachikwa mimba. Kuenea kwa ufukara kunawasukumiza wasichana wengine kuziba aibu zao na kutumia miili yao kama bidhaa ya kuuza.

Jamii ya leo inayopenda raha ina wanaume wenye ashiki za kinyama wanaowadandia wasichana wadogo na kuwabaka. Wakati mwingine huwaambukiza magonjwa ya zinaa, sikwambii kuwapachika mimba.

Mimba nyingine za wasichana wadogo hutokana na matumizi ya mihadarati. Wasichana wanaotumia dawa za kulevya hawawezi kujidhibiti wanapoteza uhalisia wao na mtazamo wao wa kimaadili. Kwa hivyo, sio mno wao kuhusika katika utovu wa nidhamu ya kingono. Wanaweza kujiingiza katika maisha yanayowaweka katika hatari ya kupata himila. Vivyo hivyo wavulana na wanaume wanaotumia dawa za kulevya wanaweza kuwashawishi au kuwashurutisha wasichana kupata mapenzi ya kiholela.

Kwa kweli dunia imebadilika sana siku hizi. Siku hizi kuna wasichana wengi wanaopachikwa mimba kabla ya ndoa kuliko enzi ya kabla uhuru. Athari ya himila hizo za mapema ni nyingi.



Wasichana wadogo hujipata wamekuwa wazazi wa watoto ingawa wenyewe wangali watoto. Jukumu la kulea vitoto vyao huwa gumu. Hali huwa mbaya zaidi wavulana waliowapachika mimba wanapodinda kuhusika au kukataa gharama ya malezi. Ndipo kukawepo watoto wengi wanaolelewa na mzazi mmoja- ambapo mara nyingi mzazi huyo mmoja tu ni mama. Baba anakuwa fumbo na tena mkimbizi mkubwa.

Wakati mwingine msichana anapopata mimba hukataliwa na wazazi wake au kukatisha masomo yake. Aidha, anaweza akaathirika kiafya kwa kubebeshwa mimba ilhali mwili wake haujakomaa vya kutosha. Maisha humgekia kuwa sawa na kukwea mlima Kilimanjaro.

a) Kwa kuzingatia mneno kati ya 65-70, fupisha mambo muhimu katika aya ya kwanza na ya pili. (Alama 9, Utiririko 1)

**Matayarisho**

..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................

**Jibu**

..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

JINA.............................................................DARASA........... NAMBARI.............

**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**Juni, 2018**
**Muda Saa 2½**

# SHULE YA UPILI YA MARANDA
# KIDATO CHA PILI, MUHULA WA PILI
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**Muda: Saa 2½**

**Maagizo:**

a) *Jibu maswali yote*

Kwa matumizi yam tahini pekee

| SWALI | ALAMA |
|---|---|
| 1 | |
| 2 | |
| 3 | |
| 4 | |
| JUMLA | |

1. **UFAHAMU** **(ALama 15)**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali***

Nchi nyingi za ulimwengu unaoendelea, au ule uliokuwa ukiitwa ulimwengu wa tatu zimegawika katika sehemu mbali mbali. Sehemu hizi zinazidi kutoshabihiana kila uchao na zinatengana kiasi cha kukaribia kupigwa mfano wa masafa ya ardhi na mbingu. Sehemu zenyewe ni mijini na mashabani. Sehemu hizi, hasa ukizitia katika **mizani** ya hali na njia za watu za maisha, zimetofautiana mno. Kiasi cha tofauti hizi ni kikubwa hadi kuonekana kama kwamba hazina uhusiano kamwe, mithili ya nchi mbili tofauti.

Hebu sasa tuzingatie yale yanayozifanya sehemu hizi kukosa kufanana. Hapa tutawajibika kuzingatia tofauti zilizo bayana baina ya watu wa shamba na wa mijini, hasa kufungamana na jinsi wanavyoyaendesha maisha yao. Jambo lililo wazi ni kwamba watu wa mashambani hawajapiga hatua ya maana kuhusu jinsi wanavyotakikana kuishi katika karne ya ishirini. Watu hawa bado wanaishi kama walivyoishi mababu zao. Hawahisi **halahala** ya jambo lolote. Mategemeo yao ni shamba; usubiriwe msimu mzuri wa mvua, watu walime, Mungu akineemeshe kilimo, wavune mavuno mema, chakula kikiwa tayari, wale, walale, siku nyingine warudie mkondo uo huo wa kuendesha maisha yao.

Watu hawa maisha yao yamepangika mikondo mitatu tu: kuzaliwa, kuoa au kuolewa, na kufa. Zaidi ya mikondo hii, maisha ya viumbe hawa hayana mabadiliko makubwa.



Mabadiliko hayapendelewi sana huko mashambani. Huko, wanaume ni mabwana, wanawake ni mfano wa vijakazi na watoto hawana tofauti kubwa na **watwana**. Mwanume akikohoa, mkewe akimbilie kulikokoholewa, na watoto watetemeke. Wanawake wa shamba na watoto hawana haki hata ya kunena, wala hawajui haki ni nini.

Kwa upande mwingine, mijini kuna viwanda, kuna majumba, kuna magari na kuna vyombo vingi sana vya maendeleo ya kisiku hizi. Watu wa mijini ni watu wa ulimwengu kote, wala si watu wa mji mmoja tu. Watu wa mji wowote ulimwenguni huweza kuwasiliana na wenzao wa miji mingine kokote kule ulimwenguni kwa njia ya rununu. Pia, kwa watu wa mjini, kuona kiumbe kidogo kabisa kisichoweza kuonekana kwa macho si shida hata. Kiumbe cha namna hiyo huonekana kupitia hadubini. Kwa wale walioondokea kuwa wanajimii wa kisasa, kuziona sayari na thurea zilizoko mbali sana nasi kupitia darubini ni jambo la kawaida sana.

Watu wa mjini huwa na mabadiliko mengi sana katika maisha yao, wala sio mikondo aina tatu tu. Kwa mfano, wanawake wa mijini hawakubali tena kuonewa na wanaume. Wanajua vyema sana maslahi yao na wameiweka jinsia yao mbele; yaani mahali pao katika jamii, wakiwa wao ni wanawake. Kupigania haki sawa na wanaume bila kulegeza kamba. Huku wakipambana kimaisha kama wapambanavyo wanaume na kufanikiwa kufanya kazi za kusikika kama vile uwakili, udaktari, uhandisi, urubani na nyinginezo zilizokuwa zikifanywa na wanaume tu. Wanawake wengine hata ni maprofesa! Kweli watu wa mijini wameendelea.

a) Sehemu zipi zimeangaziwa kama ambapo mabadiliko yanashuhudiwa katika nchi zinazoendelea? (alama 2)

.............................................................................................................

.............................................................................................................

b) Maisha ya wanaoishi mashambani yamegawika katika mikondo ipi? (alama 3)

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

c) Wanawake na watoto wanaoishi mashambani wanakandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirejelea kifungu. (alama 4)

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

d) Eleza baadhi ya mabadiliko yanayoshuhudiwa katika maisha ya watu wa mjini (alama 3)

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com